



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO
BODI YA FILAMU TANZANIA**



TANGAZO LA ZABUNI

ZABUNI NA.PA/149/2022/2023/HQ/TAFFA/N/05

ZABUNI YA KAMPUNI KWA AJILI YA SHUGHULI ZA TAMASHA LA TUZO ZA FILAMU 2022 (PROVISION OF EVENT ORGANIZING SERVICES)

1. Bodi ya Filamu Tanzania (TFB) inakusudia kutumia huduma ya kampuni katika shughuli za tamasha la tuzo za filamu mwaka 2022 linalotarajiwa kufanyika jijini Arusha.
2. Bodi ya Filamu Tanzania inapenda kuyakaribisha makampuni yenye sifa kutuma maombi yao kwa ajili ya zabuni NA.PA/149/2022/2023/HQ/TAFFA/N/05 KAMPUNI KWA AJILI YA SHUGHULI ZA TAMASHA LA TUZO ZA FILAMU 2022 (PROVISION OF EVENT ORGANIZING SERVICES)
3. Nyaraka za zabuni zinapatikana katika ofisi za Bodi ya Filamu Tanzania iliyopo 8 barabara ya Kivukoni, Utumishi, Kitalu H, S.L.P.79241, Dar es Salaam, Tanzania, Simu : +255 22 2121920, Nukushi: +255 22 2121921, barua pepe: barua@filmboard.go.tz, [Tovuti: www.filmboard.go.tz](http://www.filmboard.go.tz), nyaraka zinatolewa kuanzia saa 1.30 asubuhi hadi saa 9.30 alasiri.
4. Mwombaji atatakiwa kujaza kwa usahihi nyaraka za zabuni kwa mujibu wa maelekezo yaliyomo ndani ya zabuni.
5. Zabuni zote ziwe na nakala halisi (original) moja na nakala (copies) mbili zinazofanana, ziwekwe kwenye bahasha iliyofungwa vizuri na kuandikwa kwa usahihi "zabuni NA: PA/149/2022/2023/HQ/TAFFA/N/05" "KAMPUNI KWA AJILI YA SHUGHULI ZA TAMASHA LA TUZO ZA FILAMU 2022" na yatumbukizwe kwenye sanduku la zabuni lililopo ofisi ya Manunuzi na Ugavi Bodi ya Filamu Tanzania.
6. Mwisho wa kupokea zabuni ni tarehe 19/09/2022 Saa 5.00 asubuhi, zabuni zitafunguliwa tarehe 19/09/2022 saa 5.30 asubuhi katika ukumbi wa mikutano Bodi ya Filamu Tanzania, waombaji wote au wawakilishi wao wanaalikwa kuhudhuria ufunguzi wa zabuni hizo.

**KATIBU MTENDAJI
BODI YA FILAMU TANZANIA
DAR ES SALAAM.**